

# Kwaheri Nabhany

Machozi yanidondoka, moyoni tele huzuni,  
Habari twahuzunika, mauti yametuhini,  
Mebaki kusikitika, ametutoka Nabhani,  
Kwaheri twakutakia, ulale pema peponi.

Mechangia Kiswahili, hadhi umepigania,  
Hadi wengi mekubali, vitabu meandikia,  
Mekuwa lugha halali, juhudi tele litia,  
Kwaheri twakutakia, ulale pema peponi.

Nyoyoni tulikuenzi, wengi wetu umekuza,  
Moyoni tele mapenzi, lugha yetu kutukuza,  
Lakini leo majonzi, hofu mebaki nyamaza,  
Kwaheri twakutakia, ulale pema peponi.

Mimi matozi nalia, matoni kuwa machungu,  
Mtima kunikimbia, metangulia kwa Mungu,  
Ghafula umejifia, twasakamwa na machungu,  
Kwaheri twakutakia, ulale pema peponi.

*Ustadh Josphat Cheruiyot,  
Chuo Kikuu cha Seku, Kitui.*